**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**


**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JANETH MAGUFULI,**
S. L .P 173,
CHATO.


**Tarehe 19/04/2024.**


Simu; 0759752210/ 0763301905
janethmagufuli5@gmail.com


Kumb.Na.JMGS/ADM/F.V/*2024/2025*
**MZAZI/MLEZI WA ________________________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI** YA WASICHANA JANETH MAGUFULI **MWAKA 2024/2025 MCHEPUO WA: HGL, CBG, PCB, PCM, HGLi**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Janeth Magufuli **HONGERA SANA NA KARIBU SANA.**

## 1. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari ya Wasichana Janeth Magufuli ipo mkoani Geita wilaya ya Chato umbali wa kilometa saba (7) kutoka stendi kuu ya mabasi(KAHUMO) nauli ya pikipiki au bajaji kutoka stendi hadi shule ni TSH. 3000/=. Shule ipo kijiji cha Mbuye, jirani na Hospitali ya Rufaa , barabara ya Kasagara.

## NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA CHATO.

Kwa wanaotoka mkoa wa Kigoma, wapande magari ya kwenda Mwanza, wateremkie Bwanga au Biharamulo na hapo wapande magari ya kwenda Chato wateremkie Chato. Wanaotoka mkoa wa Kagera wilaya za; Bukoba, Karagwe na Muleba wapande magari ya kwenda Mwanza wateremkie Chato. Wanaotoka wilaya ya Ngara wateremkie Biharamulo, wapande magari ya Chato.

Kwa wanaotoka mikoa ya Mara, Arusha, Simiyu, Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro, Dar es salaam, wapande magari yanayokwenda Mwanza,wakifika Mwanza wapande magari yaendayo Bukoba wateremkie Chato. Aidha kwa njia hiyo tofauti na wanaotoka Mara, wanaweza kupanda Mabasi yanayopitia Kahama kwenda Bukoba au Geita.Vituo vya kutelemkia ni Runzewe au Bwanga.

## 2. SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.
Hivyo kwa kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii, utatakiwa kushika na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule **kwani utakuwa ukiiwakilisha shule popote utakapokuwa. Kutokujua sheria** hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki.

## 3. SARE YA SHULE

Wakati wote wa muda wa masomo mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni sketi ya dark blue kitambaa kizito na shati nyeupe (mikono mirefu) na shamba dress 2 za kitambaa kizito cha drafti ndogo rangi ya maroon (kunguru) baada ya muda wa masomo, siku za sikukuu pamoja na Jumamosi na Jumapili. Tracksuit ya kijivu itavaliwa muda wa michezo, muda wa kujisomea usiku atavaa trucksuit ya light blue(blue bahari). **Kwa sababu yoyote ile mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kuvaa nguo za kiraia(asije nazo kabisa).**

Pamoja na barua hii naambatisha viambatisho vifuatavyo.

(a) Orodha ya mahitaji,
(b) Mchanganuo wa malipo.
(c) Sheria za shule
(d) Fomu ya kukubali
(e) Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi
(f) Fomu ya mzazi/ mlezi
(g) Fomu ya hospitali

**4. KUFUNGUA SHULE**

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01, July 2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **14 July, 2024 saa kumi na moja jioni..**

**ANGALIZO; Shule haipokei fedha taslimu kiwango chochote. Malipo yote yafanyike tawi lolote la benki ya NMB au Wakala wa NMB kupitia akaunti za shule zilizotolewa katika kiambatisho (b).**

**HORTENSIA .K. DONALD**
**MKUU WA SHULE**

*Kiambatisho (a)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA WASICHANA JANETH MAGUFULI**

**MAHITAJI**
**(a) Vifaa**

- Sketi mbili dark blue zenye rinda moja kubwa mbele na nyuma na marinda madogo manne kila upande
- Mashati meupe mawili ya mikono mirefu yenye rebo ya V begani kitambaa cha rangi ya sketi.
- Tai ya dark blue
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.
- Soksi jozi mbili rangi nyeupe ndefu.
- Sweta rangi nyekundu yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni )
- T-shirt moja yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni)
- Godoro imara futi 2 ½ kwa futi 6
- Shuka 'pair' 2 rangi ya bluu na pink kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
- Chandarua ya duara 4/6 rangi nyeupe na foronya/mto rangi ya bluu.
- Ndoo moja lita 10 na ndoo moja lita 20 kwa ajili ya kuchotea maji ya kuoga na matumizi mengine na kidumu cha lita 5cheupe kwaajili ya maji ya kunywa.
- Sahani,bakuli,kikombe,na kijiko kwa ajili ya chakula.
- Yebo nyeusi isiyo na mikanda, urembo na maandishi yeyote na Kandambili kwa ajili ya kuogea **tu**.
- Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo.
- **Track suit 2 rangi, rangi kijivu na light blue yenye michilizi ya myeupe(aina ya adidas) (**zinapatikana shuleni)
- Nguo za michezo (Jezi) Bukta sizizo bana na T-sheti:- rangi Nyeusi..
- Ufagio wa plastiki wa dukani (soft bloom),ufagio wa chelewa wenye mpini kwa ajili ya usafi wa nje , raba (mopper) na ndoo yake kwa ajili ya kudekia,jembe,ndoo na kwanja.
- Ream ya karatasi nyeupe A4 (**Double A** kila muhula) kwa ajili ya mazoezi ya Darasani
- Shajala moja (file) na picha –passport size 2 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa/uraia (siyo kadi ya kliniki).
- Hati maalum ya vipimo kutoka kwa daktari kuthibitisha afya yako.
- Nakala ya taarifa ya matokeo kidato iv (result slip)
- Kikokotozi (**scientific calculator**) kwa waliochaguliwa mchepuo wa CBG, PCB na PCM
- **Dissecting kit** kwa CBG na PCB (ni lazima.). **Advanced Learner's Dictionary** HGL (ni lazima.)
- Madaftari makubwa kumi na moja(11) (counter book 3 Quires) na madaftari madogo kumi(10)
- Sanduku/Trunker la kutunzia mali zake.
- Soksi ndefu nyeusi nzito pea 2 kwaajili ya usiku.
- Kwa waislamu Ijabu na sketi ndefu, mtandio mweupe pair 2 na mweusi pair 2.
- Nguo za kuogea(taulo 1 na kitenge pair 1)
- Sabuni ya chooni lita 5
- Taa ya sola 1

**(b) Malipo**

- ✓ Mchango wa Uendeshaji Wa Shule Tsh. 65,000/=
- ✓ Tahadhari Tsh. 5,000/=
- ✓ Nembo Tsh. 5,000/=
- ✓ Kitambulisho cha Shule Tsh.5,000/=

**JUMLA . Tsh. 80,000/=**

**ANGALIZO; Shule haipokei fedha taslimu kiwango chochote. Malipo yote yafanyike tawi lolote la benki ya NMB au Wakala wa NMB kupitia akaunti za shule zilizotolewa katika kiambatisho**

***( C ) Bima ya Afya.***

Kila mwanafunzi aje na **BIMA YA AFYA** ya NHIF au shilling elfu ishirini kwa ajili ya matibabu na huduma ya kwanza.

*Kiambatisho (b)*

**MCHANGANUO WA MALIPO NA VIFAA**

**1.** Michango ifuatayo iwekwe katika akaunti ya shule inayoitwa “JANETH MAGUFULI GIRLS SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT: Ac. No. 32710025255 NMB. :

| **Na.** | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | Tsh. 65,000/= |
| 2. | Nembo ya shule | Tsh. 5,000/= |
| 3. | Tahadhari | Tsh. 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | Tsh. 5,000/= |
| | **JUMLA** | **Tsh. 80,000/=** |

**3. Vifaa vya USAFI viletwe kwa mgawanyiko ufuatavyo**:

Mzazi/mlezi unasisitizwa kukamilisha michango kwa wakati ili kuepuka usumbufu.

| **NA** | **AINA YA KIFAA** | **IDADI** | **TAHASUSI** |
|---|---|---|---|
| 1. | Ufagio wa dukani | 01 | CBG |
| 2. | Reki | 01 | |
| 3. | chelewa | 01 | |
| 4. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 5. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 6. | Mopper na ndoo yake kwa ajili ya kudekia | 01 | PCB |
| 7. | chelewa | 01 | |
| 8. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 9. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 10. | Jembe | 01 | PCM |
| 11. | Hard broom | 01 | |
| 12. | chelewa | 01 | |
| 13. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 14. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 15. | Fyekeo | 01 | HGL |
| 16. | Brush za kusuguria chooni pamoja stand yake | 01 | |
| 17. | chelewa | 01 | |
| 18. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 19. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | 01 | |
| 20. | Kotama(sickle) | | HGLi |
| 21. | Mfagio wa dukani (Soft bloom) | | |
| 22. | chelewa | | |
| 23. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | | |
| 24. | Ndoo ndogo lita 10 na kubwa 1 | | |
| | | | |

*Kiambatisho (c )*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA WASICHANA JANETH MAGUFULI**

## SHERIA ZA SHULE

### (a) TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

1. **HESHIMA**:
Kila mwanafunzi anatakiwa kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu,wazazi/walezi,wageni na viongozi kwa ujumla.
2. **MAWASILIANO**:
Kingereza ndiyo lugha pekee ya mawasiliano hapa shuleni,hivyo mwanafunzi haruhusuwi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote isipokuwa tu wakati wa midaharo ya Kiswahili.
3. **USAFI**:Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.
4. **RATIBA YA SHULE**:
Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa maalum kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii wito (**kengere.)**

### (b) MAKOSA YA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI.

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Uasherati, ushoga na ubakaji
3. Ulevi wa pombe/madawa ya kulevya kama vile mirungi,kuber,bangi n.k
4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi/walimu/jamii
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Kudharau bendera ya Taifa
7. Kubeba/kutoa mimba.
8. Kugoma,kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni /jamii
9. **Mwanafunzi kumiliki line/simu ya mkononi**
10. Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani
11. Kugomea adhabu yoyote halali
12. Kutotii serikali iliyopo madarakani na chama tawala
13. Kuwa nje ya shule bila sare ya shule na bila ruhusa/kibali maalum kutoka kwa uongozi wa shule
14. Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe
15. Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa

**ANGALIZO:Ni marufuku mwanafunzi kuja na simu. Hairuhusiwi mwalimu au mtumishi yeyote kutunza simu ya mwanafunzi.** ***Mwanafunzi atakayebainika/kukamatwa au kutumia simu tofauti na simu ya matroni atanunua umeme wenye thamani ya shilingi laki mbili tu (Tsh.200,000/=) kwenye mita namba 37248945307 –(JANETH MAGUFULI) pamoja na adhabu zingine. Hivyo mzazi hakikisha mwanao hamiliki simu kwa namna yoyote ile ili kuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima*.**

### (c) MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Utoro wa aina yoyote.
2. Kuchelewa kufika shuleni (baada ya likizo) na katika shughuli mbalimbali za shule.
3. Kutokuvaa sare rasmi ya shule kulingana na ratiba ya shule
4. Uchafu wa mwili (kutokunyoa ndevu/nywele,kutokuoga n.k ) na kutokutunza mazingira ya shule

**TANBIHI**: Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi,heater,n.k. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kumiliki redio yenye kubeba memory card/frash**. Kwa kuwa mwanafunzi harusiwi kumiliki line/simu, shule itaweka utaratibu kwa wazazi/walezi kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu 0759752210 imesajiriwa Hortensia Donald, 0766081829 Imesajiriwa Maneno Maximiliani Bishoboka, 0763301905 iliyosajiriwa kwa jina Rukia K. Selemani.**

*Kiambatisho(d)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA**
**JANETH MAGUFULI,**
**S. L .P 173,**
**CHATO.**
**Tarehe .......................**

**KUMB.NA.JMS/ADM/FV/2023/2024**

**FOMU YA KUKUBALI**

Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi) ___________________________

Mimi.................................................(mwanafunzi) bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewaya kidato cha .... katika shule ya sekondari Wasichana Janeth Magufuli. Pia nimesoma na kuelewa maelekezo yote yaliyomo katika fomu hii, naahidi kuyazingatia **yote** ikiwa ni pamoja na kutokushiriki kwa namna yoyote ile katika migomo na maanadamano yasiyoruhusiwa.

| | |
|---|---|
| ……………………… Saini ya mwanafunzi | ……………. tarehe |

Mimi…………………………………………….. mzazi /milezi wa…………………………….. (mwanafunzi) nimeyasoma masharti yote yaliyomo katika fomu ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari ya Wasichana Janeth Magufuli na ninakubali na kuahidi kwamba nitawajibika sawasawa kwa jambo lolote linalomhusu mwanagu. Aidha nitakuwa tayari kushirikiana na walimu kuhakikisha mwanangu anamaliza elimu ya kidato cha sita kwa kuwajibika kulipa michango ya shule pamoja na maelekezo megine yatakayokuwa yakitolewa na shule.

| | |
|---|---|
| ………………………….. Saini ya mzazi/Mlezi | ………………… tarehe |

*Kiambatisho ( e )*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JANETH MAGUFULI**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

***FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

1. Jina kamili ………………………………………… …………………………….
2. (a)Tarehe ya kuzaliwa………………………………… ………………………… (b)Mahali alipozaliwa…………………………………… …………………………
3.(a) Dini……………………………………………… …………………………
(b) Dhehebu……………………………………………… …………………………
4. (a) Uraia……………………………………………… ………………………….
(b) Kama siyo raia wa Tanzania taja uraia wako ……………………………………………
5. Shule ya sekondari uliyotoka………………………… …………………………………
6. (a) Jina kamili la mzazi /mlezi…………………………… ……………………………..
(b) Anwani ya mzazi/mlezi…………………………………… …………………………..
(c) Kazi ya mzazi/mlezi………………………………………… ……………………….
(d) Kituo chake cha kazi……………………………………………… …………………..
(e) Namba ya simu…………………………………………………… …………………
7. (a) Mahalia anapoishi………………………………………………… ………………….
(b) Jina la mwenyekiti wa kitongoji/mtaa ……………………………………………………
8. (a) Je, unaishi na nani?
Taja jina kamili ……………………………………………………………
(b) Je,una uhusihano gani na huyu uliyemtaja?...........................................................................
9.Ni yatima/si yatima……………………………………………………
10.Kama ni yatima mzazi yupi aliyefariki:
mama/baba/wote …………………………………………………

***Attachment (f)***

**CHATO DISTRICT COUNCIL**
JANETH MAGUFULIGIRLS SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 173,
CHATO.
Date……………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
MEDICAL OFFICER IN CHARGE
………………………………………
……………………………......…

STUDENT'S NAME...............................................................…

Please examine the above named student as to his physical/mental fitness/unfitness for admission as full time student of Janeth Magufuligirls Secondary School for academic year 2023/2024.
The examination should include the following categories: Eye sight, Hearing, Epilepsy, Urine, Venereal disease, Stool and any other body deformation

THE HEADMASTER
**RE: MEDICAL EXAMINATION RESULTS**
THE HEADMISTRESS,
JANETH MAGUFULIGIRLS SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 173,
**CHATO.**
I have examined the above student and found her with the following disease/ impairment/disabilities:
Eye sight………………………………………………………………
Urine examination……………………………………………………
Hearing ………………………………………………………………
Stool examination……………………………………………………
Speech …………………………………………………………………
Venereal diseases……………………………………………………………
Limbs……………………………………………………………………
Epilepsy…………………………………………………………………
Pregnancy test………………………………………………………..
Additional information/other serious diseases…………………………….
……………………………………………………………………………
Medical remarks…………………………………………………………….
……………………………………………………………………………
….……………………………………………………………………………………………..
Name and signature of attending officer…………..…………Date……………

Designation………………………………. Official stamp……………………

**VITABU VYA ZIADA**

Chemistry - Organic chemistry mtunzi Ngaiza
Biology- Biological science Mtunzi D. J. Taylor
Physics- Principle of physics mtunzi S. Chand
Advanced Learner's History Forms 5&6 (By Oxford)
Advanced English Dictionary
English - language for form 5and 6 (by Ndambo,S. and Kinunda,G.)
Physical Geography (By Msabila)
Practical Geography (By Zizti)








